## TIA yahamasisha amani
HABARI UK. 3

TOLEO MAALUM

# Tafakari

Kwa maamuzi sahihi

JUMATATU NOVEMBA 24, 2025

## Chanzo cha rushwa ya ngono hichi hapa

UKOSEFU wa Uwajibikaji na Uwazi katika mifumo ya chuo imeelezwa kuwa ni sababu za kuwapo kwa rushwa ya ngono vyuoni.

HABARI UK. 3

# Mwigulu: Wanaochochea uchomaji nchi wengi wao wanaishi ughaibuni



- Ataka Watanzania kuwatafakari kwa makini
- Asema wanalipwa pesa kuivuruga Tanzania

HABARI UK. 2

## Waziri Mkuu Dkt. Mwigulu aagiza mkandarasi kukamatwa, kuzuia hati
HABARI UK. 3

## Wanafunzi Singida wahimizwa kutumia mapumziko kufanya kazi kujikimu kifedha
HABARI UK. 3



## TOLEO MAALUM LA DKT. MWIGULU SINGIDA

# Mwigulu: Wanaochochea uchomaji nchi wengi wao wanaishi ughaibuni

**Na Shadrack Thobias, Singida**

WAZIRI Mkuu, Dkt. Mwigulu Nchemba, amewataka Watanzania kuwatafakari kwa makini baadhi ya watu wanaowaambia wachome nchi yetu kwani wengi wao hawapo hapa nchini, wanaishi ughaibuni na wana uraia pacha hata kama wanaongea lugha ya kiswahili.

Akizungumza na wananchi kwenye viwanja vya Bombadia Manispaa ya Singida, alisema watu wanaowashinikiza vijana kwa kuwapa pesa ili wafanye vurugu na kuchoma nchi yao, watoto wao na ndugu zao hawapo hapa nchini bali wapo katika nchi ambazo wapo.

"Hata kama mtu anaongea Kiswahili mtazame mara mbili, mapenzi yake kwa nchi ya Tanzania maana wale waliowatuma wanawapa na hela, tujiulize wanataka wanufaike na nini, wanatuambia chomeni zahanati, kituo cha afya na kuharibu barabara wakati kule wanakoishi hawaruhusu hata utupe takataka," alisema Dkt.Mwigulu.

Dkt. Mwigulu alisema vijana wa Tanzania watambue kuwa Tanzania si mali ya serikali wala ya vyama vya siasa bali ni mali ya Watanzania, hivyo tuna wajibu wa kuilinda kwani vyama vya siasa vipo kwasababu kuna nchi inaitwa Tanzania.

"Waulizeni wasio na nchi kama wana vyama vya siasa, tuilinde nchi yetu, Mungu ametupa nchi nzuri, hata hii miuondombinu si mali ya chama cha siasa na hata fedha zinazotumika kujenga miradi sio za serikali ni za watanzania,"alisema.

Dkt. Mwigulu alisema ni jambo la kushangaza kuona baadhi ya Watanzania wanakubali tu kila wanachoambiwa hata kama sio cha kweli kwa lengo la kuharibu nchi yetu.

"Zamani mkiwa mnachunga mifugo rafiki yako anakuambia leo tukifika tu nyumbani tuwapige wake zetu tuwashikishe adabu, lakini unaambiwa utumie na akili yako, wewe utaenda umpige mke wako mwenzako atakuwa anapiga ngozi kesho mwenzako ataendelea na kazi wewe umeshamvunja miguu mke wako, haya ndio ambayo yanatokea," alisema Dkt.Mwigulu.

"Nataka niwaambie Watanzania tumefikishwa pabaya watu wamejipa haki wao wamekuwa ndugu zake na Mungu na wengine wote nyie ni waongo ni wabaya, tumefikishwa pabaya Watanzania kila jambo tunakubali," alisema.

**AVUNJA UKIMYA MABASI YA ESTER**

"Siku hizi watu hawaogopi hata kusingizia jambo hafanyi hata utafiti juu ya mtu anayetaka kumsema, juzi juzi nikasikia tumechoma magari ya Ester ya mbunge wa Iramba Magharibi, magari yake yanaitwa Ester ameyaita Ester jina la mke wake,"

"Mke wangu mimi haitwi Ester anaitwa Neema, wanasema basi kama sio ya mke wake yatakuwa ya mama yake mama yangu binti wa kiislamu anaitwa Asha Ramadhani Mohamed," alisema.

"Dkt.Mwigulu alisema amezaliwa katika familia ya kifugaji ambayo huruhusiwi kufanya hata biashara ya miwa, hivyo sijawahi kufanya biashara yeyote.

Nimeingia huku serikalini kazi kubwa ninayoifanya uwekezaji mkubwa ninaoufanya ni kusomesha watoto nina kundi la zaidi ya watoto 500, nimewekeza kwenye huduma za watu," alisema Waziri Mkuu Dkt. Mwigulu.



**WAZIRI Mkuu, Dkt. Mwigulu Nchemba, akizungumza na baadhi ya mawaziri, ofisini kwake.**

# Waziri Mkuu Dkt. Mwigulu aagiza mkandarasi kukamatwa, kuzuia hati

**Na Shadrack Thobias, Manyoni**

WAZIRI Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. Mwigulu Nchemba, ameelekeza Jeshi la Polisi na Uhamiaji kuhakikisha wanamkamata na kuzuia hati ya kusafiria ya mkandarasi anayejenga mradi wa Kituo cha Ukaguzi cha Pamoja wa Magari kilichopo Kata ya Muhalala, Wilaya ya Manyoni mkoani Singida.

Dkt. Mwigulu alisema mkandarasi huyo aliaminiwa na Serikali kwa kupewa ujenzi wa mradi huo wa kimkakati uliosimama kwa zaidi ya miaka nane tangu mwaka 2016. Mradi huo unaojengwa na Kampuni ya Impresa di Costruzioni Ing. E. Mantovani S.P.A ulipaswa kukamilika mwaka 2018.

Alitoa agizo hilo mwishoni mwa wiki iliyopita alipokagua mradi huo katika ziara yake ya kikazi mkoani Singida ambapo alikagua miradi ya maendeleo na kuzungumza na wananchi.

Dkt. Mwigulu alisema kuwa jitihada zimefanyika na serikali za kuona mradi huo unaendelea, lakini mkandarasi amekuwa akileta ugumu katika utekelezaji "Mkandarasi huyu alitangazwa amefilisika na hawezi kuendelea na mradi na alielekezwa ailipe fidia Tanzania kwa sababu ameicheleweshea mradi."

"Naelekeza, Kamishna wa Uhamiaji kamata hati yake ya kusafiria, asitoke nje ya nchi mpaka jambo hili liishe, hii ni hujuma ya waziwazi, hii ni dharau ya waziwazi anaifanyia nchi yetu, Jeshi la Polisi mtafuteni mkandarasi huyu popote alipo, tumemuajiri, tunamlipa, lakini anajiamulia kama aendelee na kazi au asiendelee, huyu ni mhalifu akamatwe mpaka jambo hili liishe," alisisitiza Dkt. Mwigulu.

"Kwa taarifa nilizonazo alitangaza kwamba amefilisika kule kwao Italia na kwamba hawezi kuendelea na mradi, hata hivyo Mahakama ya Italia ikaelekeza mkandarasi ailipe Tanzania kwa sababu amechelewesha mradi, cha kushangaza zikaanza ngonjera ngonjera," alisema.

Dkt. Mwigulu alisema mkandarasi huyo licha ya kutangaza kufilisika hajataka kuachia mradi ili wakandarasi wazawa waendelee na ujenzi, hajataka kuipa nchi nafasi ya kutafuta mkandarasi mwingine atakayeweza kuendelea na mradi na pia hajataka kutoa fursa kwa Watanzania kunufanika na mradi huo.

"Amefilisika lakini ameng'ang'ania mradi huu,amesitisha mradi bila ridhaa ya serikali, ameambiwa arudishe fidia hajarudisha,nilitoa taarifa afike leo/jana eneo la mradi hajaja hii ni dharau kwa nchi yetu, ni dharau kwa waafrika, huku ni kuwahujumu vijana wa kitanzania ambao wangepata kazi hapa, huku ni kuhujumu Uchumi weti," alisema.

"Sasa naelekeza Kamishna wa Uhamiaji kamata pasipoti (hati ya kusafiria) asitoke nje ya nchi mpaka jambo hili liishe, hii ni hujuma ya waziwazi, hii ni dharau ya waziwazi,tumemwajiri, tunamlipa,amepewa fedha, amepewa kazi amejiamulia aendelee na kazi au asiendele, huyu ni mhalifu akamatwe na asitoke nje ya nchi mpaka jambo hili liishe," alisema

Dkt. Mwigulu aliwaeleza wakandarasi wa kigeni wanapokuja nchini kufanya kazi watambue kuwa Tanzania imewaajiri, hivyo sio mabosi wetu na kutoa agizo washirika ambao serikali inashirikiana nao kwenye mradi huo ndani ya mwezi huu (Novemba) jambo hili liwe limeisha na kutoa maelezo kama wataendelea na mradi huo au la.

"Hii nchi ni yetu, na mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan ametuambia hii nchi ni yetu hatuna mjomba, tuna mama yetu anaitwa Tanzania," alisema.

Aidha, Dkt.Mwigulu aliagiza mradi huo ambao ulikuwa unasimamiwa na Wizara ya Fedha, lakini kuanzia sasa uanze kusimamiwa na Wizara ya Ujenzi na kama mkandarasi huyo hataendelea tena wapatiwe wakandarasi wadogo ambao kwa muda mrefu wamesubirishwa wapatiwe ili wamalizie mradi huo.

"Huu ndio uwe mwanzo wa kuwaamini wakandarasi wazawa, hawa wanaoleta dharau kuna wengine wanatoka huko sababu nchi za Afrika zilikuwa zinatawaliwa wanapokuja wanadhani wanaenda kwenye makoloni yao, kila eneo Mungu aliumba watu wake Afrika ni yetu Tanzania ni yetu, wakija hapa tumewapa kazi wasikilize maelekezo ya nchi yetu tunayowapa,"alisema Dkt. Mwigulu.

Alielekeza wakandarasi wote wanapopewa kazi wazifanye miradi ilingane na thamani ya fedha wanazopewa na kwamba kamwe serikali haitaweza kuruhusu nchi yetu ichezewe.

Naye, Waziri wa Ujenzi, Abdallah Ulega, alisema mradi huo ni mradi wa kielelezo na una faida nyingi ambazo zitalisaidia Taifa ikiwemo kuokoa fedha nyingi zinazowekwa kwenye barabara.

"Vilevile eneo hili litakuwa ni eneo la kibiashara kwa sababu watu watapata nafasi ya kufanya biashara na wananchi kutengeneza uchumi wao, sisi Wizara ya Ujenzi tupo tayari kujenga ili mradi huo urejee" alisisitiza Waziri Ulega.



## TOLEO MAALUM LA DKT. MWIGULU SINGIDA

# TIA yahamasisha amani

**Na Shadrack Thobias, Singida**

TAASISI ya Uhasibu Tanzania (TIA) Kampasi ya Singida imewataka wanafunzi wake kujiepusha na maandamano yanayodaiwa kupangwa kufanyika Desemba 9, 2025 ambayo yamekuwa yakihamasishwa kupitia mitandao ya kijamii.

Ofisa Utumishi na Msimamizi wa Huduma za Rasilimali Watu na Utawala wa taasisi hiyo, Sanura Mohamed, alisema hayo juzi wakati akizungumza na wanafunzi wa mwaka wa kwanza (Orientation for first year student) na wa zamani kwa ajili ya kuwaelekeza na kuwakumbusha taratibu na kanuni za taasisi hiyo katika nyanja mbalimbali.

Sanura alisisitiza suala la wanafunzi kuvaa mavazi yenye staha kwani wanawaandaa kuwa watumishi wa baadae hivyo wanapaswa kuvaa mavazi yenye heshima, kuwa na nidhamu kwa jamii inayowazunguka na walimu.

Naye, Kaimu Mkuu wa taasisi hiyo, Dk. David Msokwe, alisema wanafunzi wanapaswa kuzingatia kanuni na taratibu na sheria za nchi kwani serikali kupitia taasisi hiyo jukumu lake kubwa ni kuwapa elimu hivyo ni wajibu wao kuzingatia masomo wakati wote na kufuata taratibu zilizowekwa.

"Taasisi yetu ipo kwa ajili ya kuwaandaa hivyo wakati wote mkiwa chuoni hapa muwe huru kueleza changamoto zenu kwa walimu na walezi wenu ili muweze kupata msaada," alisema Msokwe.

Mhandisi wa taasisi hiyo, Godfrey Seni, aliwata wanafunzi kutunza miundombinu ya chuo hicho kama vile samani, viyoyozi, miundombinu ya maji safi na usafi wa mazingira na kutojifanya mafundi wa kitu chochote ambacho kitakuwa kimeharibika kwani wapo mafundi kwa ajili ya kazi hiyo.

Wanafunzi hao walikutanishwa ili kuwapa uelewa kuhusu masuala ya udahili, mitihani, ulipaji wa ada, huduma za maktaba, kujisajili kupitia mfumo wa wanafunzi na kujua mazingira mbalimbali ya chuo hicho pamoja na kujua huduma zingine ambazo wanaweza kuzipata nje ya masomo.

Mambo mengine waliyoelekezwa wanafunzi hao ni masuala ya Afya ya Uzazi yaliyotolewa na Mtaalamu wa huduma rafiki kwa vijana katika Vituo vya Afya Manispaa ya Singida Dkt. Fatuma Ndoile, elimu kuhusu masuala ya mapambano dhidi ya vitendo vya rushwa vyuoni iliyotolewa na Benjamin Masyaga, Ofisa wa Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa Mkoa wa Singida.

Eneo lingine waliloelekezwa ni masuala ya sheria yaliyotolewa na mwanasheria wa chuo hicho, Wakili Joseph Wawa, masuala ya maktaba yaliyotolewa na Mkutubi wa taasisi hiyo, Joseph Mwalubanda, masuala ya ununuzi na ugavi yaliyotolewa na Mratibu wa masuala hayo wa chuo hicho, Faraji Saidi na masuala ya Dawati la Jinsia yaliyotolewa na Innocent Msumanji kutoka taasisi hiyo

## DKT. MWIGULU AKUTANA NA KATIBU MKUU WA TEC



**Waziri Mkuu, Mhe. Dkt. Mwigulu Nchemba, leo Novemba 20, 2025 amekutana na kufanya mazungumzo na Katibu Mkuu wa Baraza la Maaskofu Katoliki Tanzania (TEC), Padri Charles Kitima, katika Ofisi Ndogo ya Waziri Mkuu, Magogoni jijini Dar es Salaam.**

# Wanafunzi Singida wahimizwa kutumia mapumziko kufanya kazi kujikimu kifedha

**Na Dotto Mwaibale, Singida**

MHANDISI wa Taasisi ya Uhasibu Tanzania (TIA), Kampasi ya Singida, Godfrey Seni, amewataka wanafunzi wa taasisi hiyo kutumia muda wao wa mapumziko kufanya vibarua katika mradi wa ujenzi wa jengo la taaluma ili kujipatia fedha za kujikimu chuoni hapo.

Seni aliyasema hayo wakati akizungumza na Wanafunzi wa mwaka wa kwanza ambao wanaanza msimu wa masomo wa 2025/ 2026 'Orientasion for First Year Students' katika kikao kilichofanyika Novemba 20, 2025.

"Wanafunzi katika chuo chetu kuna mradi ambayo unafanyika baada ya Serikali kutupa fedha nawaombeni mnapokuwa kwenye mapumziko baada ya masomo njooni kufanya vibarua ili muweze kujipatia fedha za kuwasaidia badala ya kwenda kuzurura mitaani," alisema Seni.

Seni aliwaambia wanafunzi hao kuwa katika kampasi hiyo Serikali imetoa fedha Sh. Bilioni 13.5 kwa ajili ya ujenzi wa jengo la taaluma hivyo watumie fursa hiyo kwa kufanya vibarua na kujipatia fedha jambo litakalo wasaidia wazazi wao wasiangaike kuwatafutia fedha za matumizi.

Alisema jengo hilo litakuwa la ghorofa tano likiwa na kumbi za mihadhara, madarasa, kumbi za mikutano pamoja na ofisi na hadi kukamilika litatumia Sh. Bilioni 16.

Katika hatua nyingine, Seni aliwataka wanafunzi hao kuitunza miundombinu mbalimbali iliyopo chuoni hapo ili iweze kudumu na wanafunzi wengine waje waikute kama walivyo ikuta.

# Chanzo cha rushwa ya ngono hichi hapa

**Na Dotto Mwaibale, Singida**

UKOSEFU wa Uwajibikaji na Uwazi katika mifumo ya chuo imeelezwa kuwa ni sababu za kuwapo kwa rushwa ya ngono vyuoni.

Hayo yameelezwa na Ofisa wa Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) Mkoa wa Singida, Benjamini Masyaga, wakati akizungumza na wanafunzi wa mwaka wa kwanza wa msimu wa masomo 2025/ 2026 'Orientation for first year students' katika Taasisi ya Uhasibu Tanzania (TIA) Kampasi ya Singida Novemba 19, 2025.

"Pale ambapo hakuna ufuatiliaji wa walimu, taratibu za alama hazipo wazi au mawasiliano kati ya wanafunzi na uongozi ni dhaifu, rushwa ya ngono hujitokeza kwa wingi," alisema Masyaga.

Alisema vyuo vinaposhindwa kuwaadhibu hadharani wahusika, mazingira yanayotia moyo rushwa ya ngono huendelea.

Masyaga alitaja sababu nyingine inayofanya vitendo vya rushwa ya ngono iendelee ni baadhi ya wahalifu kurudi vyuoni baada ya kuhamishwa bila adhabu.

Alitaja sababu nyingine ni ile ya ushawishi kwani baadhi ya wanafunzi hasa wanaoingia chuo kwa mara ya kwanza, huathiriwa na marafiki wanaoona ngono kama njia ya kupata msaada, hivyo kupunguza uwezo wa kutambua ukatili au rushwa.

Masyaga alisema ili kuzuia na kupambana na rushwa ya ngono inatakiwa elimu na uhamasishaji kwa wanafunzi itolewe kupitia warsha za mara kwa mara.

Alieleza jambo lingine ni kuwepo kwa uadilifu wa kitaaluma, haki na wajibu wa mwanafunzi na namna ya kuiripoti rushwa ya ngono pamoja na kuanzisha kozi fupi za Ethics and Anti- Corruption kw wanafunzi wapya (Orientation)

Ofisa huyo wa TAKUKURU alitaja baadhi ya njia nyingine za kupambana na rushwa ya ngono ni kuimarisha mfumo wa uongozi na usimamizi wa chuo kwa kuanzisha taratibu za wazi na shirikishi katika utoaji wa alama, usajili, malazi, udahili, mitihani na huduma nyingine.

Alisema matumizi ya mfumo wa kidijitali (online systems) unasaidia kupunguza mwingiliano wa ana kwa ana unaoweza kuchochea rushwa.

Alitaja njia nyingine kuwa ni kuanzishwa na kuimarisha Dawati la Malalamiko kwa chuo husika kuwa na dawati huru ambalo litapokea taarifa bila ya kuvuja na wanafunzi wapewe njia salama za kuripoti na kuweka kanuni za kulinda mtoa taarifa.

Aidha, Masyaga alisema serikali ya wanafunzi iwe na mafunzo ya maadili, uwajibikaji na uongozi bora na kuweka mifumo ya uwazi katika matumizi ya fedha za wanafunzi na miradi ya serikali hiyo.



# TOLEO MAALUM LA DKT. MWIGULU SINGIDA

## DONDOO YALIYOJIRI KWENYE MKUTANO WA HADHARA WA WAZIRI MKUU DKT. MWIGULU NCHEMBA, ULIOFANYIKA KATIKA UWANJA WA BOMBADIA, MKOANI SINGIDA

● Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan anawasalimia Wana Singida na anawapongeza kwa kazi kubwa ya ujenzi wa Taifa.

● Mradi wa Reli ya Kisasa (SGR) ni wa kimkakati una manufaa kwa Taifa letu, ni uti wa mgongo wa Taifa letu, hapa Singida tutanufaika na mradi huu.

● Katika siku 100, Rais Dkt. Samia ameweka vipaumbele ikiwemo kuanza kwa utaratibu matumizi ya Bima ya Afya kwa wote, anataka jambo hili lianze haraka.

● Sisi wasaidizi tutafuatilia kwa karibu ahadi zote za Rais Dkt. Samia, tutafuatilia utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi na kufuatilia miradi yote ya maendeleo ili kuwanufaisha Watanzania.

●Watumishi wa umma wanaowasumbua Watanzania hawatakuwa na nafasi, haiwezekani mwananchi anaenda kwenye ofisi ya umma anatarajia apate ufumbuzi na huduma ila anafika pale anazungushwa, huu siyo uelekeo wa Rais Dkt. Samia anaotaka.

● Rais Dkt. Samia ametoa vitendea kazi anataka kuona Watanzania wanahudumiwa kwa ufanisi, mwananchi akifika ofisini msikilize, weka kumbukumbu kisha fanyia kazi na likikuzidi lifikishe kunakostahili.




● Mkitaka wananchi wasibebe mabango wafikieni, wasilikizeni na muwatatulie kero zao, nimeitisha taarifa kila mkoa nikipita huko nikikuta kuna mambo yasiyofaa nitachukua hatua, hatuwezi kuwa nchi ya uchumi wa kati na watu hawatekelezi majukumu yao kikamilifu.

●Tanzania ni mali ya Watanzania, si mali ya viongozi wala si mali ya vyama vya siasa, tuilinde nchi yetu, tusidanganywe kufanya vitendo visivyofaa, Mungu ametupa nchi nzuri sana.

● Tanzania hii imebarikiwa sana, tunayo madini adimu, gesi na rasilimali nyingine nyingi, tunajua haya ndiyo yanayowaumiza, Watanzania hatuna sababu ya kutofautiana, tukatae utaratibu ambao unaivunjia heshima nchi yetu, twendeni tukatatue kasoro hizi sisi wenyewe tuache nchi yetu ikiwa salama.

● Vijana na Watanzania wote tuipende na tuilinde nchi yetu, tuna mambo yanayohusu vijana, Rais Dkt. Samia ameanzisha Wizara ya Vijana ambayo itashughulikia masuala yote ya vijana.

Tafakari NewsPaper
Nyumba Na. 309 Plot 27/100 Samora
Mtaa wa Mkwepu, Dar es Salaam.
blog: http/tafakarinews.blogspot.com
E-mail: tafakarinews2016@gmail.com
Simu: 0753 737 777, Dar es Salaam
Mhariri habari: 0747354444
Biashara/Matangazo: 0767000667

Tafakari
Kwa maamuzi sahihi
USIKOSE KUSOMA GAZETI LAKO LA TAFAKARI KWA HABARI ZA UHAKIKA

# TAARIFA YA MSEMAJI MKUU WA SERIKALI

**Dar es Salaam.**

1. **Salamu**

2. **Malengo ya mkutano**

Ndugu Waandishi wa Habari tumekutana hapa leo kwa ajili ya jambo moja ambalo nimeona nimezungumze nanyi ili kueleza baadhi ya mambo yaliyojitokeza kufuatia matukio ya uvunjifu wa amani ya tarehe 29 Octoba, 2025 na siku chache zilizofuata.

Nyote mtakumbuka kuwa tarehe 29 Oktoba, 2025 ilikuwa siku ya Uchaguzi Mkuu wa Rais, Wabunge na Madiwani na Watanzania walijitokeza katika siku hii ili kutumia haki yao ya Kikatiba ya kupiga kura na kuwachagua viongozi wanaowataka.

Naomba kuchukua nafasi hii kuwapongeza Watanzania wote kwa kutumia haki hii ipasavyo na hatimaye wamempata Rais Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Wabunge na Madiwani ambao wataongoza kwa kipindi cha miaka mitano.

Halikadhalika nawapongeza kwa kujitokeza kwa wingi ambapo safari hii maandalizi mazuri yaliyofanywa na Tume Huru ya Uchaguzi Tanzania (iNEC) na kwa kuwezeshwa fedha za uchaguzi na Serikali ya Tanzania kwa asilimia 100. Tumeona Watanzania wamejitokeza kwa wingi katika kupiga kura kuliko wakati mwingine wowote na waliweza kupiga kura na kumaliza kwa haraka kwa sababu Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi ili jipanga vizuri iliandaa vituo vingi vya kupigia kura na zoezi lilikwenda kwa haraka.

**Ndugu zangu Waandishi wa Habari.**

Siku ya uchaguzi yaani tarehe 29 Oktoba, 2025 na siku chache zilizofuata kulijitokeza vitendo vya uvunifu wa amani ulioambatana na vurugu zilizokuwa zikifanywa na baadhi ya watu na ambazo zililazimu vyombo vyetu vya ulinzi na usalama kukabiliana na vitendo hivyo.

Kufuatia vurugu hizo tumepata madhara yakiwemo vifo vya raia na askari, uharibifu mkubwa wa



miundombinu ya umma na mali za watu binafsi, kuharibu biashara za watu na wizi.

Naomba kurudia kauli aliyoitoa Mheshimiwa Rais wakati akizindua Bunge la 13 la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kutoa pole nyingi kwa familia zote zilizopoteza wapendwa wao na sote tuwaombee Marehemu wote wapumzike mahali pema peponi, Amina.

Kadhalika naomba kuchukua nafasi hii kuwapa pole wote waliopata madhara mbalimbali yaliyotokana na vitendo vya vurugu zile ikiwemo kuumia, kupoteza mali zao na biashara zao, kupoteza ajira na madhara mangine ambayo siwezi kuyataja yote. Mwenyezi Mungu ayaponye maumivu yenu na inshaalah awarejeshe tena mkiwa imara.

**Tayari Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan,** baada ya kuapishwa ameunda Tume Huru ya Uchunguzi wa matukio yaliyotokea siku ya uchaguzi na siku zilizofuata. Tume hii inaongozwa na Jaji Mkuu wa Tanzania Mstaafu, Mheshimiwa Mohammed Chande Othman na itafanya kazi kwa miezi mitatu.

**Ndugu zangu Waandishi wa Habari,**

Tunapoendelea kusubiri Tume hii ifanye kazi yake na kuikamilisha, kumejitokeza wimbo kubwa la vyombo vya habari vya nje ya nchi kuchapisha na kutangaza taarifa ambazo ni za upande mmoja na wakati mwingine kufanya uposhaji wa taarifa hizo wenye mlengo wa kuchochea chuki kwa Watanzania dhidi ya Serikali, kugombanisha Watanzania wenyewe kwa wenyewe kutokana na tofauti za kisiasa, kidini na kikanda.

Naomba kurudia, Serikali ama viongozi wa Serikali akiwemo Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan inasikitishwa na imeumizwa sana na matukio yale na madhara yake. Madhara haya yametugusa sote ama moja kwa moja ama kwa namna nyingine.

Kuendelea kuyashabikia matukio yale au kuchochea kwa kutangaza na kuchapisha maudhui yenye kuzua taharuki, kupotosha ama kutia hasira watu kwa namna ambavyo vyombo vya habari vya nje ya nchi, ama wanaharakati ama watu wenye maslahi ya kisiasa wanafanya hakuna manufaa kwa Taifa letu zaidi ya kuongeza maumivu katika vidonda vya watu.

**Kutokana na hayo, kwa niaba ya Serikali naomba kueleza yafuatayo**

1. Natoa wito kwa vyombo vya habari vya nje kuzingatia maadili na misingi ya uandishi wa habari kwa kuacha kuchapisha habari za upande mmoja zenye nia ovu kwa Watanzania na nchi yetu ya Tanzania.

2. Serikali ipo tayari wakati wote kutoa ushirikiano kwa vyombo vya habari vya ndani na nje ya nchi pale watakapotaka taarifa. Naomba kusisitiza sio haki na sio sawa kwa chombo cha habari kuchapisha taarifa za upande mmoja na kisha kutoa sababu kuwa maafisa wa Serikali walitafutwa hawakupatikana kama ambavyo chombo cha habari cha CNN kimechapisha taarifa zake zilizojaa tuhuma dhidi ya Serikali ya Tanzania pasipo kutoa nafasi ya Serikali kujibu.

Kitendo kichofanywa na CNN pia kimefanywa na vyombo vya habari vingine vya Kimataifa vikiwemo BBC, Aljazeerana DW. Nasisitiza hii sio

sawa, sio haki na katika misingi na maadili ya Uandishi wa Habari huu ni ukiukwaji mkubwa n awa makusudi.

3. Kwa kuwa Rais ameunda Tume Huru ya Uchunguzi, ni muhimu vyombo vya habari vikajiepusha kuingilia uchunguzi unaoendelea na kama kuna chombo cha habari kina taarifa za uchunguzi kiwasilishe kwa Tume ili taarifa hizo zizingatiwe katika ripoti pale kamati itakapokamilisha kazi yake.

4. Kwa Waandishi wa Habari wa Tanzania na Wahariri wenzangu wa Tanzania, naomba kuwapongeza kwa kufanya kazi zenu kwa weledi, umakini na kutanguliza maslahi ya Taifa. Najua kuna magenge ya watu ambao wanashabikia nchi isambaratike yanawashambulia sana kupitia mitandao ya kijamii na vyombo vya habari vya nje ya nchi, nataka kuwatia moyo na kuwahakikishia mpo sahihi sana na mmeonyesha umuhimu wa Tanzania kwanza na upekee wa nchi yetu. Leo mtabezwa lakini historia itaandika kuwa nchi iliwahi kupita kwenye mtikisiko na Waandishi wa Habari walisimamia maslahi ya Taifa na nchi ikabaki salama.

   Endeleeni na msimamo huo. Kama nilivyosema nchi imepita katika changamoto ambazo sio nzuri kwa maslahi mapana ya Taifa. Mnachokifanya ni "Uandishi wa Habari wa Uwajibikaji" yaani Responsible Journalism – Which embarks in reporting news accurately, fair and accountable. That is verifying facts, avoiding bias and conflict of interest and being transparent about sources and mistakes

5. Kwa Watanzania wote, naomba kuchukua nafasi hii kuwasihi kujiepusha kushabikia na kusambaza taarifa ama habari zinazochochea uhasama, hasira na kuvunja umoja wetu wa Kitaifa.

   Naomba Watanzania, tung'amue mtego wa kuliangamiza Taifa letu. Tunapita kwenye kipindi ambacho tukiendekeza uchochezi unaofanywa na watu ambao wapo nje ya nchi na hawaguswi na chochote juu ya maisha yetu, wanaowashawishi vijana wetu kufanya vitendo vya kuumiza nchi yetu tutakaoumia ni sisi na tutaumia kweli tukifanya masihara.

   Ni vizuri mjue kuwa tupo kwenye kipindi ambacho kwa kiingereza kinaitwa Information Warfare (yaani Vita vya taarifa). Wasiotutakia kheri wanatumia mwanya wa upashanaji taarifa kutugombanisha, kutuchonganisha na kutufitinisha ili tukiharibikiwa waweze kupata maslahi yao, na kwa sehemu kubwa ni maslahi ya kisiasa na kiuchumi. Wanatumia mkakati unaitwa "The weaponization of narrative" yaani wanatumia silaha ya kutengeneza simulizi ya Tanzania inayoonesha Tanzania ni nchi mbaya, nchi ya hatari, nchi isiyokuwa salama na nchi isiyofaa. Wanataka wageni wakiwemo wawekezaji, wafanyabiashara na watalii waogope kuja Tanzania.

   Na naposema haya situngi maneno. Wote mtakuwa mmeona, kampeni za mtandaoni zilizoanzishwa kwa lengo kuathiri uchumi wetu, kuwatishia Watalii wasije Tanzania, Wanawatisha wawekezaji waogope kuwekeza Tanzania, Wanawatisha wafanyabiashara waogope kupitisha mizigo yao Tanzania na mengine mengi ambayo lengo lao ni kuangusha uchumi ili nchi iingie katika matatizo yatakayowaumiza Watanzania na kuwapa faida washindani wetu wa kiuchumi.

   Baadhi ya mbinu hasi wanazotumia ni kutengeneza maudhui ya uongo na kusambaza mtandaoni, mfano jana tu wametengeneza nukuu ya uongo ikinukuu mimi Msemaji Mkuu wa Serikali kwamba nimesema Mwandishi wa Habari atakayenukuu taarifa za chombo kimoja cha habari cha kimataifa na video za uchochezi, eti atashtakiwa kwa uhaini, sijasema maneno haya wametengeneza.

   Wametengeneza nukuu nyingine ya uongo ya Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan eti ameagiza Mwandishi wa Habari wa Nchi Jirani anayefanya kazi chombo kimoja cha kimataifa wakamatwe na kushtakiwa kwa uhaini.

   Nawaomba Watanzania tukatae kuruhusu mambo haya. Mheshimiwa Rais ameshasema Serikali ipo tayari kusikiliza wote wenye madukuduku, wenye ushauri na wenye maswali. Yote yatapokelewa na yatafanyiwa kazi. Hakuna sababu ya kuharibu nchi.

   Wengine wanakwenda kutengeneza uongo kuwa mifumo yetu ya malipo na akaunti za amana katika benki na taasisi za fedha sio salama. NI UONGO MTUPU na Upuuzwe.

   Natamani Watanzania mtambue kuwa malengo ya watu hawa,



kutengeneza chokochoko, kufanya uchochezi mitandaoni na kwenye vyombo vya habari, kutia hasira watu ili waharibu nchi yao na mengine ni KUANGUSHA UCHUMI WA TANZANIA, NI KUHARIBU BIASHARA ZETU, NI KUPUNGUZA WATALII ILI TUKOSE FEDHA na kibaya zaidi ni kutaka Tanzania iadhirike ili washindani wetu wa kibiashara wanufaike.

Ni muhimu kutambua hii ni vita ya uchumi, huku kwenye habari (kupitia vyombo vya habari na mitandao ya kijamii ni njia ya kupitia tu). Na tukiruhusu mtego huu tutakaoathirika ni sisi Watanzania wote.

**NAOMBA KURUDIA** kama nilivyosema awali, matukio yale yalitokea kwa siku chache na katika miji michache ya nchi yetu. Kwa sasa hali ni shwari na Watanzania wanaendelea na shughuli zao kama kawaida. Vyombo vyetu vya ulinzi na usalama vinaendelea kuhakikisha watu na mali zao wanabaki kuwa salama na matishio yote ya kiusalama yanakabiliwa ipasavyo.

Shughuli zetu za kiuchumi zinaendelea vizuri na Tanzania kwa hivi sasa ni moja ya nchi chache ambazo zinakwenda kupiga hatua kubwa za kiuchumi kupitia miradi mikubwa na ya kimkakati inayoendelea na mingine imeanza kukamilika na kutoa huduma

**Miradi kama;**

i. SGR – Kazi inaendelea vizuri sana, kwa vipande vyote nane vya kuanzia Makutupora – Tabora, Tabora – Isaka, Isaka – Mwanza, Tabora – Kigoma na Kigoma kwenda Burundi.


Sasa hivi tupo katika maandalizi ya ujenzi wa reli mpya (tunakwenda kujenga njia ya Kaskazini {Tanga-Arusha-Musoma kilometa 1,028), njia ya Kusini {Mtwara -Mbambabay kilometa 1,000}.

Pia tunakamilisha maandalizi ya kuanza ujenzi wa treni za mjini zitakazopita juu katika Majiji yetu tukianza na Jiji la Dar es Salaam {zijulikanazo kama Mono Rail} tumepanga kuanza na Kawe, Mwenge, Mlimani City, Ubungo, kisha tunaelekea Kariakoo na kuunganisha na SGR. Tutakuwa na tawi jingine la Bibi Titi kwenda Morocco kupitia barabara ya Ali Hassan Mwinyi, kisha tunaunganisha Mwenge. Hii awamu ya kwanza na kila kilometa 2 tutaweka Kituo. Lengo tujenge mtandao wa kilometa 160.

Tutakuwa na treni hizi za Mjini pia katika Jiji la Dodoma ambapo tumepanga kujenga kuanzia stesheni ya SGR kwenda Mjini, kisha tutaunganisha kwenda Mtumba hadi Chamwino kupitia Stendi ya Mabasi. Awamu ya pili tutaelekea Msalato Airport. Lengo kwa Dodoma tujenge kilometa Mtandao wa kilometa 105

ii. Uboreshaji wa Bandari yetu ya Dar es Salaam na jinsi tulivyojipanga kufikia nchi Jirani za Kongo (DRC), Burundi, Rwanda, Uganda, Zambia, Malawi.

Wote mmeona ufanisi katika bandari



yetu ya Dar es Salaam umeongezeka maradufu na kuwa tishio kubwa kwa washindani wetu hasa baada ya Serikali kuamua kushirikiana na DP World ambapo sasa uwezo wa bandari kuhudumia mizigo umeongezeka maradufu kutoka kuhudumia tani Milioni 21 mpaka tani Milioni 32 ndani ya miaka 3 mapato ya bandari pia yameongezeka kutoka shilingi Bilioni 900 hadi zaidi ya shilingi Trilioni 1.8 hivi sasa. Meli zinashusha kwa haraka zaidi (muda wa meli kusubiri umepungua kutoka siku 46 hadi 7) na gharama za uendeshaji wa bandari zimeshuka na tunaokoa zaidi ya shilingi Bilioni 400 ikilinganishwa na kabla ya DP World.

Na mengine mengi mfano wote juzi tu tumeshusha meli ya 1 kati ya meli 4 tunazojenga katika ziwa Tanganyika {Hizi zinakwenda kuongeza biashara kubwa kati ya Tanzania na Kongo – mzigo uliokuwa unazunguka kupitia nchi Jirani utakuwa unatoka Tanzania kwenda Kongo moja kwa moja. Tumejipanga hadi mwaka 2029 tufikie kuhudumia tani Milioni 50 ikilinganishwa na sasa tunahudumia tani Milioni 32 ambazo zimeongezeka kutoka kwenye matarajio ya tani Milioni 28

Lakini pia tumefanya makubwa katika bandari zetu za Tanga na Mtwara. Kule Mtwara tunajenga bandari Kisiwa Mgao ambayo itahudumia mizigo yote iitwayo Dirty Cargo (Mfano Makaa ya Mawe, Saruji, Chuma, Klinka n.k)

Tanga tumeboresha bandari kwa kuongeza gati mbili na sasa meli nyingi zinapita Tanga, hata zile zilizokuwa zinapita bandari Jirani sasa zinapita Tanga. Tulikuwa tunahudumia tani laki 4 na sasa tunahudumia tani Milioni 1.5 (Mwaka huu tutafika tani Milioni 2). Uwezo wa Bandari yetu ya Tanga sasa ni tani Milioni 3 kwa mwaka. Na tunajenga gati nyingine 3 na kituo cha kupokelea mafuta

Halikadhalika tumekamilisha bandari ya Bukoba na Kemondo. Bandari ya Mwanza North nayo tunaikamilisha manaake mzigo wa Uganda utapita Tanzania (sasa hivi tunahudumia asilimia 3 tu, baada ya hapo tutaongeza hadi asilimia 38)

Bandari ya Bagamoyo, tunaanza kujenga Desemba hii 2025. Mitandao ya ujenzi ipo njiani na bandari hii itakuwa na kina cha hadi mita 20 na itakuwa na uwezo wa kupokea meli kubwa kuliko bandari za ukanda

huu wa mashariki. Tutajenga gati 28 (tutaanza na gati 14). Bandari itakuwa na uwezo wa kuchukua meli zenye uwezo wa kubeba makontena hadi 25,000. **TUJIULIZE NANI ATAKAYEPENDA?**

Pia tumeanza kujenga Bandari ya Kigoma na mkandarasi yupo Site. Tutaongeza uwezo wake mpaka kufikia tani milioni 3 ikilinganishwa na sasa ambapo inahudumia tani laki 6.

Na mkumbuke miradi hii yote inakwenda kuajiri vijana wetu kwa maelfu na watapata kipato kizuri. Na tunajipanga kumwaga ajira kama mchele.

iii. Kwenye utalii ndio usiseme, tuliweka lengo la kuongeza Watalii kufikia Milioni 5 hadi mwaka 2025, tumefanikiwa kuongeza hadi zaidi ya Watalii 5.3. Na sasa tumeanza safari ya kufikia Watalii Milioni 8. Watalii hawa wanapoongezeka kwetu maana yake wanapungua kwa washindani wetu.

iv. Shirika letu la ndege (ATCL) limeimarika sana. Sasa hivi tuna ndege 16 na kati ya sasa na 2030 tunakwenda kununua ndege zingine 8. Sasa hivi tunahudumia vituo 29, kabla ya mwisho wa mwaka huu tunaongeza vingine 3 ambavyo ni Cape Town (Afrika Kusini), Accra (Ghana) na Victoria Falls (Zimbabwe). Hadi mwaka 2030 tutafika vituo 50 vya ndani na nje ya nchi.

Kwa upande wa abiria sasa hivi tunahudumia abiria 1,500,000 na tunapanga kufika abiria 3,000,000 katika miaka miwili ijayo. Miaka minne iliyopita tulikuwa tunasafirisha abiria kama 800,000 tu kwa mwaka.

v. Uchumi wetu halikadhalika, unakuwa vizuri. Mwaka huu tunapanga ukue kufikia wastani wa asilimia 6

vi. …..

Ni vizuri Watanzania wajue kuwa mafanikio haya ya bandari yanawaathiri washindani wetu, na kwa hiyo **HATUWEZI KUPENDWA, TUTASHAMBULIWA TU.**

Na tunaposhambuliwa namna hii, tunakwenda kuathiriki kama nchi na pia kwa mtu mmoja mmoja. Bandari zikiathirika tutakosa mapato, tutashindwa kununua dawa, kujenga barabara, kusambaza maji, kusambaza umeme kugharamia elimu, afya na mengine. Utalii ukianguka na sisi wananchi tutakosa ajira, Mama lishe watakosa biashara, madereva wa taxi wataathirika na ajira zitapotea.

**TUAMKE WATANZANIA**

6. Kwa watalii (To our prestigious tourists), these are the few words from the government;

i. Welcome to the United Republic of Tanzania. Our nation remains peaceful, calm, and open to all who wish to explore its beauty—from Kilimanjaro and the Serengeti to Ngorongoro, Dar es Salaam, and Zanzibar to mention a few. Please ignore any misinformation meant to distract you from the unforgettable experiences awaiting you here.

ii. Our destinations are safe, our accommodations are improving every day, and our hospitality and transportation ensure that your journey is comfortable and memorable.




iii. The government is fully committed to protecting you, your companions, and the value of your dollars and shilings while visiting our country.

7. Mwisho, jana nilitoa tangazo kwa umma baada ya chombo cha habari cha CNN kuchapisha makala ya matukio ya tarehe 29 Oktoba, 2025. Kwanza uhakiki wa maudhui yaliyomo katika makala ile unaendelea lakini kama ambavyo chombo hiki kimefanya katika ripoti zake mbalimbali kimeendelea kufanya makosa ya kiweledi na kiuadilifu katika uandishi wa habari kwa kutangaza na kuchapisha maudhui ambayo yanaegemea upande mmoja. Sio kweli kwamba CNN ilishindwa kupata upande wa Serikali kwa ripoti zao zote wanazotoa.

Inashangaza kwa chombo cha habari cha kimataifa kama CNN kufanya makosa makubwa ya kimaadili kama haya ambayo yamefanywa. Serikali inatoa wito kwa CNN kuzingatia maadili na weledi katika uandishi wa habari na kujiepusha na uchapishaji wa taarifa zisizokuwa na vyanzo halali na rasmi, kupotosha na kuzua taharuki. Najua mwandishi wa habari wa CNN aliyeandaa makala ile hakuwa Tanzania na ameandaa makala kwa kutumiwa picha zilizopigwa kwa simu wakati wa vurugu na bila kuwasiliana na mamlaka zinazohusika Tanzania amekwenda kuandaa makala ya upande mmoja. Tusingependa tufikie kuwapa majina ambayo baadhi ya waliowakwaza wamewapa, waje tuwape upande wa Serikali na wakachapishe taarifa zenye usawa, ukweli na zisizo na mgongano wa kimaslahi. Waache kuchagua kuripoti upande mmoja wakati upande mwingine upo na haujawanyima taarifa.

Baada ya kusema hayo naomba kurudia kuwahakikishia Watanzania na watu wote Dunia kuwa Tanzania ni salama, Tanzania imetulia, watu wanaendelea na shughuli zao kama kawaida na yalitokea wakati wa Uchaguzi Mkuu yanachunguzwa na matokeo yake yatafanyiwa kazi.

Waandishi wa Habari wenzangu tuendelee kuilinda nchi yetu kwa wivu mkubwa, maendeleo tunayopata sasa wapo ambao yanawakwaza na watatafuta kila njia ya kutuangusha TUKATAE.



# TOLEO MAALUM LA DKT. MWIGULU SINGIDA









Waziri Mkuu, Dkt. Mwigulu Nchemba alipokagua maendeleo ya ujenzi wa Kituo cha Ukaguzi cha Pamoja cha Magari kilichopo kata ya Muhalala Wilaya ya Manyoni mkoani Singida.



# Dkt. Mwigulu Nchemba

Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania

GREEN ARMY 2025 - 2030 FOR EVERYBODY

## MAISHA YA AWALI

- Alizaliwa tarehe 7 Januari 1975, katika Kijiji cha Makunda, Wilaya ya Iramba, Mkoa wa Singida, Tanzania.
- Alisoma Shule ya Msingi Makunda (1987-1993).
- Elimu ya Sekondari, alihudhuria Shule ya Sekondari Ilboru (O-Level) na baadaye Shule ya Sekondari Mazengo (A-Level) Jijini Dodoma.
- Ametoka katika familia ya kawaida Kijijini, lakini alisoma kwa bidii na kufaidika na mikopo ya wanafunzi kufikia elimu ya juu

## ELIMU

- Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM)
- Shahada ya Kwanza ya Uchumi (2001 - 2004)
- Shahada ya Uzamili ya Uchumi (2004-2006)
- Shahada ya Uzamivu (PhD) katika Uchumi (2012-2018)
- Cheti cha Uongozi kutoka Taasisi ya Uongozi (Uongozi Institute, 2002).

## SAFARI YA KISIASA

**Ndani ya CCM na Bungeni**

- Ni Mwanachama wa Chama Cha Mapinduzi (CCM).
- Mbunge wa Jimbo la Iramba Magharibi kuanzia mwaka 2010 Hadi hivi sasa.
- Mweka Hazina wa CCM (2011-2012)
- Naibu Katibu Mkuu wa CCM (2012-2015).

## WIZARA ALIZOHUDUMU

- Waziri wa Kilimo, Mifugo na Uvuvi (Novemba 2015-Juni 2016)
- Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi (Juni 2016 - Julai 2018)
- Waziri wa Katiba na Sheria (Mei 2020 - Machi 2021)
- Waziri wa Fedha na Mipango (Machi 2021 - Novemba 2025)

## UWAZIRI MKUU TANZANIA

- **Tarehe 13 Novemba 2025,** Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan alimteua Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba kuwa Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

@greenarmy_2025

#GreenArmy4Everybody
#KaziNaUtuTunasongaMbele



# TOLEO MAALUM LA DKT. MWIGULU SINGIDA









**Mkuu wa wilaya ya iramba Suleiman Y. Mwenda ameshiriki hafla maalumu iliyoandaliwa na Waziri Mkuu Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Nchemba katika kijiji cha Makunda, wilaya ya Iramba mkoani Singida. Hafla hiyo imejikita katika kuhimiza Amani maendeleo ya wananchi na kuimarisha ushirikiano kati ya Serikali na jamii.**

Tafakari
MICHEZO
Jumatatu Novemba 24, 2025

# Dkt. Mwinyi aipongeza Yanga SC






**Na Mwandishi Wetu**

Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Mhe. Dkt. Hussein Ali Mwinyi, ameipongeza Klabu ya Young Africans Sports Club kwa ushindi wa bao 1 - 0 dhidi ya AS FAR Rabat kutoka Morocco, katika mchezo wa michuano ya Ligi ya Mabingwa Afrika uliochezwa leo kwenye Uwanja wa New Amaan Complex, Zanzibar.

Amesema kuwa ushindi huo umewapa heshima ya kipekee na kuandika ukurasa mpya katika historia ya michezo nchini, huku Young Africans ikionesha ubunifu wa hali ya juu na mchezo uliokomaa ambao umeleta ushindi mkubwa.

Dkt. Mwinyi amesema kuwa Serikali itaendelea kushirikiana na wadau wa michezo nchini ili kuhakikisha mazingira ya michezo yanaimarika zaidi, hatua itakayoongeza uwezo wa timu kuwa na ushindani mkubwa katika mashindano ya Kimataifa.

Aidha, Rais Dkt. Mwinyi amewashukuru Mashabiki na Wananchi wote waliojitokeza na kuipa nguvu Young Africans SC, akieleza kuwa umoja na hamasa walizozionesha leo umeufanya Uwanja wa New Amaan Complex kuwa sehemu ya historia katika kukuza michezo nchini.